Jina ______________________ Nambari ya usajili ______________

Shule __________________________ Tarehe ______________

Maagizo: JIBU MASWALI YOTE MUDA: SAA 1 DAK 40

**ZOEZI 1: INSHA (AL 20)**

**Endeleza insha ifuatayo:**

Ilikuwa siku ya Harambee. Mipango yote ilikuwa imekamilika..........................................

SEHEMU YA B:

ZOEZI 11: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

2. Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali.

Sungura, Fisi, Tumbili na Kobe ni wanafunzi wa shule ya upili ya Mwituni. Huko ndiko walikokwenda shule kila siku. Siku moja, Sungura alijificha na kwenda kula miwa ya jirani yao Bwana Nyati. Nyati alimlalamikia mwalimu Simba kwa kusema, "Wanafunzi wako ndio wanaopitia shambani mwangu wakila miwa"

Mwalimu Simba aliwaita wanafunzi wote na kuwakanya. Kobe alimshuku Sungura ndiye mwizi wa miwa. Aliamua kumtega Sungura. Aliona miwa miwili iliyokuwa imekomaa vizuri. Alijua bila shaka Sungura angeitamani miwa hiyo. Kobe alipaka miwa hiyo gundi ikametameta. Alijificha kwenye miwa. Punde Sungura alifika. Aliangalia huku na kule. Alijisemea, "Si kawaida kupata miwa ya kupendeza kama hii. Lazima ni mitamu kama asali. Hapa ndipo pahali pangu."



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

Sungura aliushika muwa mmoja ili auvunje. Mkono wake wa kulia ukanata. Alishika muwa wa pili kwa mkono wa kushoto, ukanata. Alilia kwa sauti. Sauti ilisikika kwa mbali Kobe alijitokeza na kushangaa, "Kumbe Sungura ndiwe mwizi wa miwa ya Bwana Nyati? Kwa hakika siku za mwizi ni arubaini." Nyati aliwasili mara moja. Sungura alijua yu mashakani. Nyati alimwangalia Sungura kwa macho makali. Sungura alitetemeka kwa uoga na aibu. Alimwomba Nyati msamaha. Aliahidi kumpandia Nyati miwa mingine. Nyati alimsamehe Sungura kwa masharti makali.

(a). Taja wahusika wanne katika hadithi hii. (al 2)

________________________________________

(b). Eleza sifa mbili za Sungura zinazojitokeza katika hadithi hii. (al 4)

(i). ________________________________________

(ii). ________________________________________

(c). Taja fani mbili ya lugha iliyotumika katika hadithi hii. (al 2)

(i). ________________________________________

(ii). ________________________________________

(d). Wanafunzi walikuwa wakisoma katika shule ya upili iliyoitwaje (al 1)

________________________________________

(e). Unajifunza nini kutokana na hadithi hii? (al 2)

________________________________________

(f). Kisawe cha aibu ni (al 1)

________________________________________

3. **Soma habari hii kisha ujibu maswali (Alama 10)**

Dawa za kulevya ni kitu chochote kinachoathiri hali ya kawaida ya mwili wa binadamu. Kuna aina mbalimbali za dawa za kulevya. Dawa hizi ni kama vile: bangi, kokeini, madraksi, heroini na ukaputi (anaesithesia). Aidha sigareti, pombe na gundi ni dawa za kulevya zinazouzwa na watu wengi pasipo kufikiria madhara yake.

Pia kuna dawa zinazopendekezwa na daktari ili kupunguza maumivu au uchungu mwilini. Zinapotumiwa vibaya, huleta **uraibu** unaoweza kuathiri afya ya mtumiaji.

Watu tofauti tofauti hutumia dawa za kulevya kwa sababu zinazohitilafiana. Kuna wale wanaotaka kudadisi dawa hizi, kuiga mienendo ya marafiki zao na kukinaishwa na maisha. Wengine huzitumia kwa kuwa hawana shughuli za kufanya, wameathiriwa na vyombo vya mawasiliano hasa runinga na uozo wa jamii.

Matumizi ya dawa hizi kwa muda mrefu husababisha uzoefu ambao ni vigumu kuukatiza. Hivyo basi, huleta madhara mengi yasiyo na kifani. Miongoni mwa madhara haya ni kukosa makini masomoni na kazini; aidha ukija, saratani ya mapafu hasa kwa wavutao sigara,wao hufanya uhalifu ili kugharimia dawa hizi ghali na kudhoofisha uamuzi wa kiakili unaosababisha hasara kuu.

Wakiwa katika hali hii ya kutojijua, kutojitambua, wengi huweza kujidunga kwa sirinji chafu zinazoweza kusababisha hata UKIMWI! Hatari kubwa zaidi huwa kifo ambacho ndicho hatima ya wengi washikao njia hii.

Hata hivyo, yanawezekana kuyaepuka madhara yote haya endapo sote tutawajibika kwa kukataa kuandamana na marafiki wabaya, wapotofu, kukataa kutumiwa na walanguzi wa dawa hizi na kutafuta uraibu unaofaa na kuheshimu mali yetu.

Mwito basi ni kushirikiana bega kwa bega ili kujaribu kuangamiza dawa za kulevya na biashara yake.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

(a). Eleza maana ya dawa za kulevya. (al 2)

______________________________________________

______________________________________________

(b). Taja mifano miwili ya dawa za kulevya. (al1)

(i). ______________________________________________

(ii). ______________________________________________

(c). Dawa za kulevya zinazouzwa na watu wengi ni (al 2)

______________________________________________

(d). Uzoefu wa dawa za kulevya ni (al2)

______________________________________________

(e). Hatima ya wanaotumia dawa za kulevya ni (al1)

______________________________________________

(f). Toa sababu mbili zinazofanya watu kutumia dawa za kulevya. (al1)

______________________________________________

(g). Ipe habari hii kichwa kinachofaa. (al 1)

______________________________________________

**USHAIRI**

**4. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali (alama 10)**

Hima jamani shuleni, mbio mbio tujiunge,
Sote shime masomoni, kwa elimu tujijenge,
Bidii hasa tieni, elimu ije wafaa,
Ubaguzi uwe hakuna, ule ule wa jinsia.

Iwapo hapo nyumbani, kazi zote zifanyike,
Pasi na kubagueni, wa kiume au kike,
Tujue na tupikeni, barobaro na banati
Ubaguzi uwe hakuna, ule ule wa jinsia.

Haki iwe ni uwezo, sote nafasi tupewe,
Halio siwe kigezo, ya kazi upewe wewe,
Awe mwana au binti, apewe mwenye uwezo,
Ubaguzi uwe hakuna, ule ule wa jinsia.

(a). Andika kibwagizo cha shairi hili (al 2)

______________________________________________

(b). Ubeti wa pili una mizani ngapi? (al 2)

______________________________________________

(c). Ubaguzi unaendelezwa vipi? Eleza (al 2)

______________________________________________

(d). Shairi hili ni la aina gani? Eleza (al 2)

______________________________________________

(e). Ni lipi lengo la mshairi katika shairi hili ? (al 2)

______________________________________________



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi | Tel:+254202319748 E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com